# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

NYALANJA HIGH SCHOOL
P.O BOX 141
MEATU
EDUCATION FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYALANJA HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU MKOA WA SIMIYU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

+255757-296046/ +255712-679143/ +255762-017052

Shule ya sekondari Nyalanja,

S.L.P 141,

**MEATU – SIMIYU.**
**Tarehe…………………………………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………………………..**

**S.L.P …………………………………….**

**Yah: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA……….KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYALANJA HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU MKOA WA SIMIYU MWAKA …………..</u>.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha………..katika Shule hii mwaka ………………….. na atasoma tahasusi ya **HKL/HGK/CBG** (kata isiyohusika). Shule ya Sekondari Nyalanja ipo umbali wa Kilometa 48 Kusini - Magharibi mwa Mji wa Meatu.

**USAFIRI.**

- Ukiwa Shinyanga panda gari la **SHINYANGA- MWABUZO** nauli ni Tsh 8000/=.
- Ukiwa Meatu panda gari la **MEATU – MWABUZO** nauli ni Tsh 4000/=, **MWABUZO – NYALANJA** nauli ni Tsh 2000/= kwa pikipiki.
- Ukiwa Mwanza panda gari la **MWANZA – MEATU** nauli ni Tsh 13000/=, utalala Meatu, kesho yake panda gari la **MEATU – MWABUZO.**
- ukiwa Bariadi panda gari la **BARIADI – MEATU** nauli ni Tsh 8000/=, utalala Meatu, Kesho yake panda gari la **MEATU – MWABUZO**
- ukiwa Igunga panda gari la **IGUNGA – MWABUZO** nauli ni Tsh 10000/=.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

**2.1. Sare za Shule**

i. Sketi mbili (2) za rangi ya bilinganya kwa ajili ya darasani (iwe ndefu usawa visigino) yenye linda kubwa mbele na nyuma, pembeni malinda madogo madogo;

ii. Mashati mawili (2) rangi nyeupe yenye mikono mirefu (tetroni);

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni rangi nyeupe kwa ajili ya darasani na maji ya bahari (light blue) kwa ajili ya kushindia, ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama;
iv. Sare ya michezo ni Track suit jozi moja (1) rangi ya blue na raba jozi moja (1) nyeupe (sport shoes);
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi ndefu jozi mbili (2) rangi nyeupe;
vii. Sweta la shule rangi ya dark blue;
viii. Magauni mawili (2) (shamba dress) rangi ya maji ya bahari (light blue) mshono wa gauni solo linalofunika visigino.
ix. Tai mbili (2) rangi ya bilinganya;
x. Tisheti (T-shirt) rangi ya dark blue yenye kola nyeupe na nembo ya shule.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari counter book Q4, jumla nane (8) na kalamu za kutosha;
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa kila mwaka wa masomo;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi ya HKL, HGK na CBG orodha ya vitabu imeoneshwa uk. 7 & 8;
iv. Godoro la futi mbili na nusu (2.5);
v. Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu na pinki, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1;
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Hard broom 1 (HKL, HGK), jembe 1 (HKL, HGK na CBG), squezer 1 (CBG), mifagio 2 wa
x. Ndani (CBG) na nje(HKL, HGK).

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha zote zilipwe kupitia akaunti ya shule Na **30901100010** benki ya **NMB**, jina la akaunti **NYALANJA SECONDARY SCHOOL** (Isipokuwa, **Nembo** na **Kitambulisho** pamoja na **Tahadhari**, zilipwe kwa mhasibu wa shule). Stakabadhi ya benki iletwe kwa mhasibu wa shule. Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye **Bank Pay Slip (BPS)**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;

vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**TANBIHI:**

Mwanafunzi hatapokelewa shuleni endapo hatakamilisha mahitaji muhimu ya shule yalioyoelekezwa kwenye fomu hii. Njoo na mahitaji pamoja na michango yote ili kuepusha usumbufu. Vilevile mwanafunzi aje na **CHETI CHA KUZALIWA (BIRTH CERTIFICATE) na RESULT SLIP (original na copy).**

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

--------------------------

SALOME S. GULENGA

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NYALANJ
MEATU

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- Mkuu wa shule: +255757-296046/ +255712-679143
- Makamu Mkuu wa Shule: +255762-017052/ +255717-569110
- Mwandamizi Taaluma: +255689-599167/ +255688-384584
- Mwandamizi Malezi: +255784-819752

**ORODHA YA VITABU**


ENGLISH LANGUAGE 1 & 2.

- Asheli, N. (2018): Advanced level English Language. Structure & Stylistics. Dar es salaam APE NETWORK.
- Ndambo, S.G & Kinunda, J.E (2017): Advanced level English Language 1. Form 5 & 6. Dar es salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

LITERARY BOOKS.

- **Plays**
  - "Betrayal in the City – Francis Imbuga"
  - "An Enemy of the People – Henrik Ibsen"
  - "Lwanda Magere – Okoiti Omtatah"
  - "The Bride – Austin Bukenya"
  - "I Will Marry When I Want – Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Mirii"

- **Novels**
  - "A Man of the People – Chinua Achebe"
  - "His Excellency the Head of State – Danny Safo"
  - "The Beautyful Ones Are Not Yet Born – Ayi Kwei Armah"
  - "Vanishing Shadows – Namige Kayondo"
  - "Divine Providence – Severine N. Ndunguru"

- **Poetry**
  - "Selected Poems – Institute of Education"
  - "The Wonderful Surgeon and Other Poems – Charles Mloka"

HISTORY 1 & 2.

- Tumaini, S.C.K (2017): Contemporary Historical Events Vol.1 Advanced Level History 1. Dar es salaam: Che Guevara Investment.
- Yassin, S: Essentials in Advanced Level History paper 1. Dar es salaam: Ahmadiyya Printing press
- Yassin, S.: Essentials in Advanced Level History paper 2. Dar es salaam: Ahmadiyya Printing press

KISWAHILI 1 & 2.

- Masebo J.A. & Nyangwine N.C.M (2018): Nadharia ya Lugha Kiswahili 1. Kidato cha 5 & 6. Dar es salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Taasisi ya Elimu Tanzania (2016): Kiswahili Kidato cha Tano Fasihi. Dar es salaam TIE.FASIHI YA KISWAHILI.

1. Riwaya
   - Mfadhili – Hussein Tuwa
   - Usiku Utakapokwisha – Mbunda Msokile
   - VutaN'kuvute – Shafi Adam Shafi
   - Kufikirika – Shaaban Robert

2. Tamthiliya
    - Morani – Emmanuel Mbogo
    - Nguzo Mama – Penina Muhando
    - Kivuli Kinaishi – Saidi A. Mohamed
    - Kwenye Ukingo wa Thim – Ebrahim Hussein

3. Ushairi
    - Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu
    - Kimbunga – Haji Gora Haji
    - Chungu Tamu – Theobard A. Mvungi
    - Mapenzi Bora – Shabaan Robert

GENERAL STUDIES (GS).

- Bigirwamungu, J. & Deogratias, S.M. (2019): Understanding General Studies for Advanced level. Dar es salaam: APE NETWORK

GEOGRAPHY 1 & 2.

- Masabila, Physical geography
- Masabila, Practical geography
- Masabila, Human geography

BIOLOGY 1 & 2.

- Biology for Advanced Secondary Schools, TIE
- Biological Science

CHEMISTRY 1 & 2.

- Chemistry for Advanced Secondary Schools, TIE

BASIC APPLIED MATHEMATICS

- Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary Schools, TIE

NYAKAHANJA HIGH SCHOOL P.O BOX 141 MEATU EDUCATION FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT

**PRIME MINISTER'S OFFICE -TAMISEMI**

NYALANJA SECONDARY SCHOOL

P.O. BOX 141

MEATU – SIMIYU

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by a Medical Officer)

Student's name ……………………………………………………………………….....

Age ………………………………………………………………………………………

Blood count (red and white) ……………………………………………………

Stool ……………………………………………………………………………………

Urine ………………………………………………………………………………….

Syphilis Test ………………………………………………………………………….

T.B Test …………………………………………………………………………….

Eyes Test ……………………………………………………………………………

Ears Test ……………………………………………………………………………..

Chest ………………………………………………………………………………

Spleen ………………………………………………………………………………

Pregnancy Test ………………………………………………………………….

Any additional information, e.g. Physical defects, chronic or family diseases etc

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

I certify, the above student is Fit/Not Fit to pursue further studies

Signature ………………………………………………….

Designation …………………………………………….

Station ………………………………………………….

Date ………………………………………………….....

**FOMU YA MZAZI NA MWANAFUNZI KUKIRI MAKUBALIANO (AHADI ZA UTII).**

Ijazwe kwa herufi kubwa na irudishwe kwa mkuu wa shule.

A. TAARIFA ZA MWANAFUNZI.

Jina kamili: ______________________________________________________
Tarehe ya kuzaliwa: _______________________________________________
Shule uliyotoka: __________________________________________________
Kijiji/Mtaa uliozaliwa: ____________________________________________
Kata: _____________________________________________________________
Wilaya: ___________________________________________________________
Mkoa: ____________________________________________________________
Uraia: ____________________________________________________________
Dini: _____________________________________________________________
Kabila: ___________________________________________________________

B. TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI.

jina la mzazi/mlezi: _______________________________________________
Namba ya simu: ___________________________________________________
Mahali anapoishi: _________________________________________________
Kazi ya mzazi/mlezi: _______________________________________________

C. AHADI YA MWANAFUNZI.

Mimi ______________________________________________________. Nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria za shule. Nayakubali na niko tayari kuwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Nyalanja. Nitatimiza masharti yote ya shule na sheria za shule. Nikikiuka ahadi zangu nichukuliwe hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Tarehe __________________________________ sahihi ya mwanafunzi ___________________.

D. AHADI YA MZAZI/MLEZI.

Mimi _____________________________________________________ (Mzazi/mlezi) wa mwanafunzi _______________________________________________. Nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote kwa mwanafunzi huyu.

Hivyo, naahaidi kwamba

a) Nitashirikiana kikamilifu na uongozi mzima wa shule katika kuelimisha na kumlea ipasavyo.
b) Nitatimiza mahitaji yake yote ya shule.
c) Sitamkatiza masomo kwa minajiri ya shughuli za kifamilia, kumuozesha na mambo mengine kama hayo.
d) Nitafanya kila jitihada kumwezesha mwanangu kuwahi shule kila siku na kufika shule siku ya kufungua shule bila kuchelewa.

Tarehe ___________________________. sahihi ya mzazi/mlezi _________________________.



T-SHIRT YA SHULE



SHAMBA DRESS



SARE YA DARASANI



SARE YA DARASANI KWA WAISLAM

NYALANJA HIGH SCHOOL
P.O BOX 141
MEATU
EDUCATION FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT